

## Ruzuku ya Ulezi wa Watoto

Mei 2008

Mpango wa Ruzuku ya Ulezi wa Watoto husaidia kulipa gharama ya ulezi wa mtoto. Husaidia aina nyingi za familia. Hizi ni pamoja na zifwatazo:

- Familia ambazo zinapokea TAF ( Msaada wa Muda wa Familia) – Mpango huu husaidia familia kupata na kutunza kazi.
- Familia zinazofanya kazi, za mapato ya chini.
- Familia zingine katika shughuli za elimu au mafunzo – Hii inatoa usaidizi wa kutunza kazi au kupata kazi nzuri.
- Wazazi wa vijana wanaomaliza chuo cha upili au GED.

### Ili kustahili, familia lazima zifanye zifwatazo:

Ikiwa mzazi/mlezi/ mtoa huduma anahitaji ulezi wa watoto, mpango huu unaweza kutoa msaada wa kifedha. Watu lazima waombe na waweze kuchukua hatua kwa niaba yao wenyewe. Familia hiyo na mtoto huyo lazima waishi Kansas. Lazima watoe habari zote za mapato. Ikiwa wazazi hawako nyumbani, yule aliye nyumbani lazima afanye kazi na Watoa huduma ya Kuwasaidia Watoto.

Mtoto lazima awe chini ya umri wa miaka 13. Ikiwa mtoto aliye na umri wa miaka 13-18 hawezi kujilea, anaweza kustahili msaada katika kesi zingine. Wafanyakazi wanazingatia ustadi wa kujilinda kimwili na kiakili. Koti ikimwangaia mtoto, anaweza kustahili usaidizi.

### Habari ya mapato:

Wafanyakazi watazingatia mapato ya kila mwezi kwa kila mmoja wa familia. Mapato hayo ni pamoja na mishahara kabla ya ushuru na msaada wa mtoto. Wafanyakazi hawahesabu mapato mengine. Mifano ni pamoja na SSI na Mikopo ya Wanafunzi.

Ikiwa mapato ya familia yanafikia viwango vya mpango, wanaweza kustahili msaada wa ulezi wa watoto. Familia hutumia msaada huu ili kugharamia gharama ya ulezi kutoka kwa mtoa huduma waliyemchagua wa kulea watoto. Familia nyingi lazima zilipie sehemu ya gharama ya ulezi wa watoto. Viwango vya msaada vinatofautiana kifamilia msingi ukiwa hali za kesi za kibinafsi.

Maongozi ya upeo wa mapato ya kila mwezi ni kama yafwatayo:

- Ukubwa wa familia ya 2 -\$2,159
- Ukubwa wa familia ya 3 -\$2,714
- Ukubwa wa familia ya 4 -\$3,269
- Ukubwa wa familia ya 5 -\$3,824
- Ukubwa wa familia ya 6 -\$4,379
- Ukubwa wa familia ya 7 -\$4,934
- Ukubwa wa familia ya 8 -\$5,489
- Ukubwa wa familia ya 9 -\$6,044
- Ukubwa wa familia ya 10 -\$6,599
- Ukubwa wa familia ya 11 -\$7,154
- Ukubwa wa familia ya 12 -\$7,709

## **Watoa huduma ya Ulezi wa Watoto:**

Wazazi huchagua watoa huduma ya ulezi wa watoto kutoka kwa aina zifwatazo:

- Kituo kilichoidhinishwa cha ulezi wa watoto
- Nyumba ya familia iliyoidhinishwa ya ulezi wa watoto
- Nyumba ya kikundi kilichoidhinishwa cha ulezi wa watoto
- Nyumba iliyosajiliwa ya ulezi wa watoto
- Jamaa ya mtoto (mtoto huenda kwa nyumba ya jamaa)
- Mtoa huduma kuja kwa nyumba ya mtoto

Ikiwa mtu anamlea mtoto wake mwenyewe, SRS haitatoa msaada. Pia, ikiwa mtoa huduma anaishi kwenye kaya, SRS haitatoa msaada. Watoa huduma lazima wajiandikishe na SRS ili wastahiki malipo kutoka kwa wazazi. Lazima waweze kupokea malipo kielektroniki (pesa kuwekwa moja kwa moja) kwa akaunti ya benki.

**Watoa huduma wanaohibitwa wanaotaka kujiandikisha na SRS ili kutumikia familia zinazosaidiwa wanapaswa kupigia simu 1-888-369-4777 au ofisi ya mtaani ya SRS.**

## **Vile Wazazi Wanavyolipa**

Msaada wa ulezi wa watoto hutolewa kwa familia zinazotumia Kadi ya Vision ya uhawilishaji wa Manufaa Kielektroniki (EBT). Ni sawa na kadi ya matumizi. Fedha na Msaada wa Chakula pia hutolewa kupitia kadi ya Vision. Msaada huwekwa katika akaunti ya ulezi wa mtoto kwenye kadi ya Vision kila tarehe moja ya kila mwezi. Familia hutumia msaada huu ili kuwalipa watoa huduma kielektroniki kwa mwezi.

Shirika la Fedha za elektroniki (eFunds Corporation) ndilo kontrakta wa EBT kansas. Hao uhawilisha pesa kwa akaunti ya benki ya mtoa huduma wakati familia inapouliza. Watoa huduma lazima wajiandikishe na Shirika la Fedha za elektroniki (Efunds Corp.) ndiposa kupata malipo.

## **Habari zaidi:**

Kwa habari zaidi juu ya Mpango wa Ruzuku ya Ulezi wa Watoto:

- Enda kwa [www.srskansas.org](http://www.srskansas.org)
- Piga simu 1-888-369-4777
- Chukua fomu za maombi katika Ofisi yoyote ya SRS/ Eneo la Ufikiaji